USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

# TOLEO MAALUM LA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) KWA WANANCHI

**AGOSTI, 2015**

**Wajibu na majukumu**


Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na pia imefafanuliwa zaidi kifungu Na.10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

**Dira**

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

**Dhamiri**

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.




**Katika kutoa huduma zenye ubora na tija, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

| | |
|---|---|
| **Kutopendelea** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki. |
| **Ubora** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma. |
| **Uadilifu** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria. |

| | |
|---|---|
| **Zingatio kwa Wadau** | Tunalenga matakwa ya wadau wetu kwa kujenga utamanduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi. |
| **Ubunifu** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi. |

## UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahimiza umuhimu wa upashanaji habari miongoni mwa wanajamii. Ibara ya 18 (2) inasema: "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii." Pia, Taasisi ya Kimataifa ya Ukaguzi (INTOSAI) inahimiza juu ya haki ya wananchi kujua masuala ya kisera yenye tija kwenye maisha yao.

Kwa kuzingatia matakwa hayo ya Kikatiba, kisheria na kitaaluma, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) imekuwa ikiandaa kwa mwaka wa tatu sasa kitabu hiki chenye lengo la kuibua umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa kaguzi mbalimbali zinazofanywa na Ofisi yangu. Dhima ya kijitabu hiki ni kuwa chachu miongoni mwa wananchi katika kujijengea tabia ya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo zinazotekelezwa na Serikali.

Ni dhamira yangu kuendelea kushirikisha jamii na wadau mbalimbali katika kufanikisha majukumu niliyonayo ya Kikatiba katika kuhakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinatunzwa na kutumiwa kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za utawala bora, hivyo kuhakikisha kunapatikana maendeleo ya haraka kwa wananchi wote.

Ni imani yangu kuwa taarifa zilizochapishwa zitaongeza ufanisi na uwajibikaji kwa shughuli za Serikali kwa lengo la utekelezaji wa miradi na hatimaye kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Kama ilivyo ada, napenda kulishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi yake nzuri wanayoifanya ya kusoma ripoti za ukaguzi kwa lengo la kusimamia vizuri Serikali. Nitumie fursa hii kuishukuru Serikali na kuwashukuru watumishi wote wa Serikali kwa kutupatia ushirikiano mzuri wakati wote wa ukaguzi. Pia, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wafadhili mbalimbali wanaoendelea kuisaidia Ofisi yangu kwa misaada mbalimbali wanayoitoa ikiwemo ya kifedha, kitaaluma na vitendea kazi.

Kipekee, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kujitoa kwao katika kuwatumikia Watanzania. Natambua juhudi zao katika kuandaa taarifa kwa kuzingatia weledi wa hali ya juu zenye tija kwa Taifa letu. Nawaomba waendelee kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza malengo ya kuanzishwa kwa Ofisi yetu na maendeleo ya Taifa letu.

Prof. Mussa J. Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**
Agosti, 2015

## DIBAJI

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kifungu Na. 34(1)(c) cha Sheria Na. 11 ya ukaguzi wa umma ya mwaka 2008, inataka Ripoti za ukaguzi zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu nza serikali kuwasilishwa bungeni.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa kitabu hiki cha muhutasari wa ripoti za ukaguzi wa hesabu na ufanisi kwa mwaka 2013/2014 ambacho ni toleo maalum la tatu kwa ajili ya wananchi.

Ili kupunguza upotoshaji na kufanikisha mjadala wa masuala ya taarifa za ukaguzi nimeona nifanye jitihada za kuelimisha umma wa Watanzania ili uweze kuelewa na kuchambua masuala ya ukaguzi kwa usahihi kulingana na mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu. Jitihada hizo ni pamoja na kuandaa kitabu kidogo kinachoelezea muhtasari wa ripoti hizo.

Lengo kuu la kutoa kitabu hiki ni kuwawezesha wananchi pamoja na wadau wengine kupata taarifa zilizowasilishwa Bungeni mwaka huu kwa lugha rahisi na rafiki zaidi ambayo kila mdau anaweza kuielewa na kuitumia. Njia hii itachangia kupanua wigo wa upatikanaji na usomaji wa ripoti zilizotolewa bila ya upotoshaji na hivyo kufikisha ujumbe sahihi kwa jamii.

Pia, kitabu hiki kinalenga kutoa majumuisho ya muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha na ufanisi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2014, kutoka Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Ufanisi pamoja na Kaguzi Maalumu.

Ni matarajio ya Ofisi yangu kuwa Bunge na wawakilishi wengine wa Wananchi wakiwemo Madiwani watatumia taarifa hizi kiusahihi katika kutekeleza majukumu yao ya usimamizi wa fedha za umma na utoaji huduma kwa wananchi.

Dhamira ya Ofisi yangu ni kuendelea kutoa kitabu hiki ili kiweze kukidhi matakwa ya wasomaji na watumiaji. Hivyo Ofisi inakaribisha maoni ili kuboresha taarifa zetu na kitabu hiki kwa siku zijazo.

**YALIYOMO**

**Kurasa**


Wajibu na majukumu ........ i
Dira ........ i
Dhamiri ........ i
UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ........ iv
DIBAJI ........ v
YALIYOMO ........ vi
SURA YA KWANZA ........ 1
1.1 UTANGULIZI ........ 1
1.2 HAKI YA MWANANCHI YA KUPATA TAARIFA ........ 1
1.3 RASILIMALI ZA UMMA ........ 1
1.4 UWAJIBIKAJI ........ 1
SURA YA PILI ........ 2
2.1 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI ........ 2
2.2 HATI ZA UKAGUZI ........ 2
SURA YA TATU ........ 4
UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YALIYOTOLEWA MIAKA ILIYOPITA ........ 4
3.0 UTANGULIZI ........ 4
3.1 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA KAGUZI ZA FEDHA ZA MIAKA YA NYUMA ........ 4
3.2 MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI ........ 4
3.3 MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA ........ 5
SURA YA NNE ........ 7
4.1 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU ........ 7
4.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2013/2014 ... 7
SURA YA TANO ........ 14
5.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA ........ 14
5.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA ........ 14
SURA YA SITA ........ 20
6.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA ........ 20
6.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA ........ 20
SURA YA SABA ........ 25
MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO ........ 25
7.0 UTANGULIZI ........ 25
7.1 MATOKEO YA UKAGUZI ........ 25
**Fedha iliyopokelewa** ........ 25
SURA YA NANE ........ 31
8.0 MUHTASARI WA RIPOTI ZA KAGUZI MAALUM ........ 31
8.1 MATOKEO YA UKAGUZI MAALUM ........ 31
SURA YA TISA ........ **Error! Bookmark not defined.**
UKAGUZI WA UFANISI ........ **Error! Bookmark not defined.**
9.0 UTANGULIZI ........ **Error! Bookmark not defined.**
9.1 USIMAMIZI WA MIPANGO MIJI ........ **Error! Bookmark not defined.**
9.2 MAKISIO YA MAHITAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA MUHIMU . **Error! Bookmark not defined.**
9.3 UKARABATI WA MAJENGO YA SERIKALI ........ **Error! Bookmark not defined.**


9.4 UTOAJI WA HUDUMA ZA UGANI KWA WAKULIMA ........................ **Error! Bookmark not defined.**
9.5 UTEKELEZAJI WA MIFUMO YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA KWENYE SEKTA YA MADINI .. **Error! Bookmark not defined.**
........................................................................................................ **Error! Bookmark not defined.**
SURA YA KUMI ........................................................................ 46
10.0 MAONI MAALUM YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ... 46
10.1 Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa......... 46
10.2 Changamoto kuhusiana na uanzishwaji wa Halmashauri Mpya...................... 46
10.3 Mahitaji ya kurekebisha kifungu cha 38(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 ............................................................**Error! Bookmark not defined.**

## SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

## 1.2 TAARIFA ZA UKAGUZI

Kwa mujibu wa Kanuni ya 8(5) ya Kanuni za sheria ya fedha za mwaka 2001 (iliyorekebeshwa 2004), kila Wizara, Wakala na Idara za Serikali inajukumu la kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu shughuli na rasilimali za taasisi hiyo zinatolewa kwa umma. Hivyo basi taasisi hizo zinapaswa kuandaa na kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa za mwaka za bajeti, malengo na mipango ya kila programu, tathimini ya utekelezaji wa malengo, muhutasari wa matokeo ya taarifa za fedha kama ilivyoidhinishwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, pamoja na mipango ya miaka miwili inayofuata kama ilivyoidhinishwa na Bunge.




Hivyo napenda kusisitiza kuwa wananchi wana haki ya Kikatiba na Kisheria ya kupata taarifa sahihi zinazohusu uendeshaji wa taasisi za umma. Hivyo ni wajibu kwa kila mwananchi kutafuta taarifa zilizotajwa hapo juu ili kuweza kufanya tathimini ya utendaji wa taasisi hizo.

## 1.3 RASILIMALI ZA UMMA

Rasilimali za Taifa zinajumuisha fedha, maliasili ya nchi, watu, ardhi na mambo mengine yote yanayohitajika katika uendeshwaji wa Serikali kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Uwajibikaji katika rasilimali za Taifa ni dhana ya maadili na utawala bora.

## 1.4 UWAJIBIKAJI

Ni dhamana ambayo wanapewa watu au taasisi katika kusimamia na kuzilinda

rasilimali za Umma kikamilifu na kuwa tayari kuwajibika kwa maamuzi waliyoyafanya. Kuna mihimili mikuu mitatu ya uwajibikaji nchini ambayo ni:

**Bunge**

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Wananchi lina wajibu wa kuidhinisha na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali.

**Serikali:**

Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, zina wajibu wa kukusanya na kutumia rasilimali za Umma kama zilivyopitishwa na Bunge.

**Mahakama:**

Mahakama, inawajibu wa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria husika za nchi.

## SURA YA PILI

### 2.1 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya ukaguzi Na 200(ISA 200),lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Taasisi Wizara, Idara, Mashirika ya Umma na Halmashauri,kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango vya mfumo unaokubalika.

### 2.2 HATI ZA UKAGUZI

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayotolewa na mkaguzi baada ya kujiridhisha kama taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya taaluma ya uhasibu na vile vya bodi ya uhasibu na ukaguzi Tanzania. Aina ya hati za ukaguzi zinazotolewa ni kama ifuatavyo:



### 2.2.1 Hati inayoridhisha

Hati hii hutolewa pale ambapo Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kuzingatia viwango husika.

### 2.2.2 Hati yenye shaka

Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonyesha vizuri hali ya kifedha isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa.

### 2.2.3 Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha hazikuandaliwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika.

### 2.2.4 Hati mbaya

Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni kuhusiana na hesabu hizo.

## SURA YA TATU

## UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YALIYOTOLEWA MIAKA ILIYOPITA

### 3.0 UTANGULIZI

Sura hii inatoa taarifa ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa fedha na wa ufanisi yaliyotolewa kwa miaka iliyopita.

### 3.1 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA KAGUZI ZA FEDHA ZA MIAKA YA NYUMA

Mapendekezo ya ukaguzi yamegawanyika katika makundi matatu ya utekelezaji, yaani ya muda mfupi, ya muda wa kati na ya muda mrefu. Katika kupitia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi niliyoyatoa miaka iliyopita, jumla ya mapendekezo 77 yalitolewa kwa Serikali, ambapo jumla ya mapendekezo 16 sawa na asilimia 21 ya mapendekezo yaliyotolewa yalifanyiwa kazi kikamilifu na mapendekezo 26 sawa na asilimia 34 yanaendelea kufanyiwa kazi na mapendekezo 35 sawa na asilimia 45, utekelezaji wake upo katika hatua za awali za utekelezaji kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 1: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa mwaka 2013/2014**

| Na. | Ripoti | Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaendelea | Mapendekezo ambayo utekelezaji wake upo katika hatua za awali |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Serikali Kuu | 26 | 0 | 20 | 6 |
| **2** | Serikali za Mitaa | 25 | 0 | 10 | 15 |
| **3** | Mashirika ya Umma | 31 | 2 | 16 | 13 |
| **Jumla** | | **77** | **16** | **26** | **35** |

### 3.2 MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ulifanyika kwa ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi zilizowasilishwa Bungeni ambazo ni:

(i) Kuzuia na Kudhibiti Athari za Mafuriko ya mwaka 2007;

(ii) Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi ya mwaka 2009;

(iii) Programu ya ukaguzi wa Shule za Sekondari Tanzania ya mwaka 2009;

(iv) Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu katika Miji Mikubwa na mikoa ya mwaka 2009; na

(v) Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara ya mwaka 2010.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo katika ripoti hizo, umebaini kuwa kati ya mapendekezo 110 ya ukaguzi wa ufanisi yaliyotolewa, mapendekezo 49 (sawa na asilimia 45) yalitekelezwa, mapendekezo 42 (sawa na asilimia 39) utekelezaji wake unaendelea na mapendekezo 19 (sawa na asilimia 16) utekelezaji wake bado haujaanza kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali Na 2 hapa chini;

**Jedwali Na.2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi tano za Ufanisi**

| Na. | **Mapendekezo** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Jina la Ukaguzi** | **Yaliyotekelezwa Kikamilifu** | **Yanayoendelea Kutekelezwa** | **Ambayo haya jatekelezwa** | **Jumla** |
| i. | Kuzuia na Kudhibiti Athari za Mafuriko | 10 | 6 | 3 | 19 |
| ii. | Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi nchini | 9 | 10 | 1 | 20 |
| iii. | Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari nchini | 6 | 5 | 1 | 12 |
| iv. | Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu katika Miji Mikubwa na Mikoa nchini | 11 | 6 | 12 | 39 |
| V | Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara Tanzania | 13 | 5 | 2 | 20 |
| **Jumla** | | **49** | **42** | **19** | **110** |
| **Asilimia** | | **45** | **39** | **16** | **100** |

## 3.3 MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

### Idadi ya kaguzi zilizofanyika

Katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2014, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya ukaguzi katika Halmashauri 163, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali 176, Mashirika na Taasisi za Umma 109, Miradi ya Wafadhili ikiwemo; ASDP, TASAF, WSDP, HBF, Global Funds na mingineyo inayotekelezwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Ukaguzi wa Miradi umetoa jumla ya ripoti 755. Pia nimefanya ukaguzi wa ufanisi na kutoa Ripoti 5. Aidha, nimefanya kaguzi maalum 17 katika Halmashauri 6, Wizara 8 na Mashirika ya Umma 3. Hivyo kwa ujumla Ofisi imefanya jumla ya kaguzi 1,245 kwa mwaka 2013/2014.

### Hati zilizotolewa

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014, nimetoa jumla ya Hati za Ukaguzi 1,223 (bila kujumlisha kaguzi maalum 17 na za ufanisi 5). Kati ya hati hizo, hati zinazoridhisha ni 1,124 (92%), hati zenye shaka 94 (7.5%), hati zisizoridhisha 5 (0.5%) na hakukuwa na hati mbaya. Pamoja na kwamba kuna jumla ya hati zisizoridhisha tano kwa taasisi zote nilizokagua kwa mwaka huu, mwelekeo wa hati za ukaguzi, kwa ujumla zinaonyesha kuimarika kwa utendaji

wa Serikali ikilinganishwa na miaka iliyopita. Ufuatao ni mchanganuo wa Idadi ya Hati zilizotolewa kwa mwaka huu:

**Jedwali Na. 3: Muhtasari wa Hati zilizotolewa Mwaka 2013/2014**

| Na. | Taasisi zilizokaguliwa | Idadi ya Taasisi zilizokaguliwa | Aina ya hati za ukaguzi | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Hati zinazoridhisha | Hati yenye shaka | Hati isiyoridhis ha | Hati mbaya |
| 1 | Wizara, Idara na Taasisi zake | 176 | 166 (94%) | 1 (0.5%) | 1 (0.5%) | 0 (0%) |
| 2 | Halmashauri | 163 | 150 (92%) | 13 (8%) | 0 (0%) | 0 |
| 3 | Mashirika ya Umma | 109 | 105 (96%) | 4 (4%) | 0 | 0 |
| 4 | Miradi ya Maendeleo | 775 | 703 (92%) | 68 (9%) | 4 (0.5%) | 0(0%) |
| | **Jumla** | **1,223** | **1,124(92%)** | **94(7.5%)** | **5 (0.5%)** | **(0.0%)** |

Misingi ya aina ya Hati za Ukaguzi zilizotolewa hapo juu imefafanuliwa kwa kina katika ripoti husika. Nakala za ripoti hizo zinapatikana katika Ofisi zote za Taifa za Ukaguzi na pia kupitia kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ( www.nao.go.tz ).

## SURA YA NNE

## 4.1 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Wizara na Idara za Serikali sitini (60), Sekretarieti za Mikoa ishirini na tano (25), wakala wa serikali thelathini na mbili (32) Mifuko maalum kumi na mbili(12), Balozi thelathini na nne (34), taasisi nyinginezo kumi na tatu (13) na Vyama vya siasa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2014.

## 4.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2013/2014

### 4.2.1 Utekelezaji wa bajeti

Ukaguzi uliofanyika kuhusiana na bajeti umebaini mapungufu katika utekelezaji wa bajeti kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 4: Mapungufu yanayohusiana na bajeti ya Serikali kuu**

| Maelezo | Fedha za makusanyo ya mapato (TZS Bilioni) | Fedha za matumizi ya kawaida kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali (TZS Bilioni) | Fedha za matumizi ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali (TZS Bilioni) |
|---|---|---|---|
| Makadirio | 17,887.83 | 9,959.81 | 5,035.94 |
| Fedha zilizopokelewa/kukusanywa | 16,304.29 | 9,559.55 | 3,147.03 |
| Fedha zisizopokelewa/zisizokusanywa | (1,583.54) | 400.26 | 1,888.91 |
| Fedha zisizopokelewa/zisizokusanywa kwa asilimia | (8.85) | 4 | 38 |


### 4.2.2 Upungufu katika hesabu za Majumuisho za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

- Kujumuishwa kwa Taasisi zenye kutumia kanuni za Uhasibu tofauti kutokana na uwepo wa sera mbalimbali za kihasibu katika taasisi za umma.kunapelekea kuleta uwalakini wa uhalisia wa taarifa za hesabu za majumuisho.

- Uandaaji wa Hesabu za majumuisho kwa kutumia Taarifa ambazo hazijakaguliwa hupelekea hesabu za majumuisho kugubikwa na tofauti kubwa kati ya taarifa zake na zile hesabu za serikali na taasisi zake. Kwa sababu hiyo, taarifa za Hesabu za Majumuisho zinaweza kutokuwa sahihi.
- Kushindwa kujumuisha Uwekezaji wa Serikali kwa wabia wanne na wakala (Associates) 27 katika hesabu za majumuisho ambapo kunaweza kupelekea taarifa za fedha za Majumuisho kutokuelezea hali halisi.

**4.2.3 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania**

- Mamlaka ya Mapato ina kesi za muda mrefu katika bodi ya rufaa ya kodi na mahakama ya rufaa zenye thamani ya  Shilingi trilioni 1.72. ambazo kiasi cha shilingi bilioni 261.19 zimekwama katika Mahakama ya Rufaa na kiasi kilichobaki cha shilingi trilioni 1.46 kinasubiri maamuzi katika bodi ya rufaa za kodi. Hali inaiongezea serikali gharama na hasara za undeshaji wa kesi na pale mrufani atakapofilisika kabla ya kesi kuamuliwa.




- Mafuta yenye msamaha wa kodi ya shilingi bilioni 22.33 yaliyokusudiwa kutumika migodini katika kampuni ya Geita Gold Mines na Resolute Tanzania Limited yalihamishwa kwenda kwa kampuni isiyostahili misamaha.
- Upotevu wa kiasi cha shilingi milioni 392.7 uliosababishwa na kampuni ya Kiliwarrior Expedition Ltd ya Arusha iliyokuwa imesamehewa kodi kufanya matumizi mabaya ya misamaha kwani baadhi ya magari yalisajiliwa na kutumiwa na watu wasiostaili msamaha huo.
- Kukosekana kwa ushahidi wa uondokaji nchini wa mali zenye kodi ya jumla ya shilingi bilioni 835.97 iliyoagizwa kupitia nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine. Mali hizo zinaweza kutumika nchini na kuikosesha serikali mapato ya kiasi hicho cha fedha.

- Kutokukusanywa kwa ada ya mchakato wa forodha (Customs Processing fees) kutoka kampuni ya Gesi ya Uingereza (BG Company) yenye jumla ya shilingi milioni 511.50.
- Misamaha maalum ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ilitolewa kwa kampuni ya Swala Oil and Gas(T) Ltd mara mbili kwenye Ankara moja ya dola za kimarekani 326,078 (sawa na shilingi milioni 540.60)
- Kodi iliyokokotolewa ya shilingi bilioni 33.15 haijakusanywa kwa muda mrefu kutokana na udhaifu katika mfumo wa ukusanyaji wa kodi katika ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania katika mikoa ya Kinondoni, Ilala, Temeke na Mwanza.
- Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi kilichopaswa kulipwa kwa shilingi bilioni 28.53 na fedha za kimarekani 329,149(sawa na shilingi bilioni 29.08) kutokana na kutokuwepo kwa mfumo wa kutosha wa upitiaji makadirio ya kiasi cha kodi na hivyo kupelekea kuinyima serikali mapato .

### 4.2.4 Msajili wa Hazina

- Serikali kuchelea kuongeza mtaji kwenye mashirika na taasisi inazowekeza wakati ilipohitajika kufanya hivyo na kupelekea hisa za serikali kupungua au kuwa katika hatari ya kuisha kabisa. Hii imedhihirika katika hisa za Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Biashara (NBC 1999 Ltd), Shirika la Ndege (ATCL), TAZARA, TTC na Shirika la Reli (TRL) ambayo yote yalikumbwa na uhaba wa mtaji.
- Kutozingatiwa kwa misingi ya utawala bora hasa katika uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi na watendaji wakuu. Kwani baadhi ya Bodi bado zina wabunge na wafanyakazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, jambo hili linaleta mgongano wa maslahi.

### 4.2.5 Deni la Taifa

- Serikali imetoa udhamini wa mikopo kwa taasisi za serikali kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Bunge. Udhamini wa mikopo hiyo umekuwa ukiendelea pasipo kuingizwa katika Deni la taifa. Vilevile, serikali imekuwa ikifanya malipo ya mikopo kwa taasisi zilizokiuka masharti ya udhamini. Mikopo hiyo bado imeendelea kutoingizwa katika hesabu za deni la taifa.
- Serikali ilipanga kukopa kwa kuuza dhamana zenye thamani ya shilingi trilioni 1.90 kwenye soko la ndani ili kuendesha bajeti ya serikali na pia kugharamia dhamana zilizokomaa. Badala yake, serikali iliuza dhamana zenye thamani ya shilingi trilioni 3.17 sawa na ongezeko la asilimia 66.4. Ongezeko la ukopaji lina athari kubwa katika utekelezaji wa bajeti kwani

serikali inalazimika kutenga pesa zaidi kwa ajili ya kugharamia dhamana hizi kwa kulipa riba na gharama nyingine ambazo hazikuwa katika bajeti.

### 4.2.6 Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Pensheni

- Ukokotoaji usio sahihi wa mafao ya wastaafu uliopelekea majalada 355 kuzidishwa kwa kiasi cha shilingi milioni 982.51 na majalada 283 kupunjwa shilingi milioni 281.46. Hii inaonyesha umuhimu wa ukaguzi wa awali katika malipo ya mafao ya wastaafu, kwani pasipo kufanyika serikali ingepoteza jumla ya shilingi milioni 701.06.
- Ucheleweshaji usiokuwa na tija katika kuandaa mafao ya wastaafu. Uchelewesha huu umepelekea baadhi ya wastaafu kushindwa kuandaliwa malipo yao na pia kuigharimu serikali tozo (penalty).
- Malimbikizo ya michango kutokana na taarifa zenye makosa za waajiriwa ya shilingi milioni 299.98. Ujazaji usio sahihi wa taarifa za watumishi unaofanywa na Maafisa Masuhuli unapelekea serikali kuingia kwenye gharama zisizostahili na pia kuwanyima watumishi stahiki zao za mafao wanapostaafu.

4.2.7 Udhaifu katika usimamizi wa raslimali watu na taarifa za mishahara

- Malipo ya shilingi milioni 141.39 yaliyohusisha taasisi saba (7) za umma yalifanywa kwa watumishi waliostaafu, waliofukuzwa na walioacha kazi ambao hawakugundulika na kuondolewa kwenye orodha ya mishahara kwa wakati.




- Wizara na Idara tisa (9) Sekretarieti za mikoa 14 na balozi sita (6) ambazo idadi ya watumishi waliotakiwa katika ikama ilikuwa 18,027 lakini zinawatumishi 8,359 waliopo kazini na kusababisha upungufu wa watumishi 8,359. Upungufu huu wa watumishi unaathiri utendaji wa Serikali katika utoaji wa huduma

- Wizara ya maji, sekretarieti ya mkoa wa Rukwa na Njombe hazikurejesha Hazina fedha za mishahara kiasi cha shilingi milioni 121.84 ambazo zilikuwa ni mishahara isiyolipwa. Kutorejesha kwa mishahara isiyolipwa kwa muda mrefu kunaweza kusababisa matumizi mabaya ya fedha hizo.
- Serikali ililipa malipo ya posho na kodi ya nyumba kwa watumishi waliostaafu na wasio na mikataba waliopo balozini jumla ya shilingi milioni 543.79.

**4.2.8 Mapungufu katika utendaji wa Wakala wa Serikali**

- Ucheleweshwa wa fedha za miradi toka serikalini kiasi cha shilingi milioni 523.9. Hii hupelekea kutotekelezwa ama utekelezaji wa kiasi kidogo wa miradi ya maendeleo.
- Mali zenye thamani ya shilingi milioni 697.34 zilinunuliwa na wakala tatu (3) ambazo ni Wakala wa Uandikishaji wa Vizazi na Vifo Tanzania (RITA),Wakala wa Maabara za Seikali (GCLA) na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) lakini hazitumiki hivyo kutokuwa na thamani ya fedha.
- Wakala kumi (10) zilikuwa na malipo yenye nyaraka pungufu ya kiasi cha shilingi bilioni 1.83 na wakala tisa (9) zilikuwa na masurufu ya yasiyorejeshwa kiasi cha shilingi milioni 724.55.
- Shule ya Sheria ya Tanzania ilikuwa na limbikizo la deni la shilingi bilioni 7.58 mwishoni mwa Juni 2014 lililotokana na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa shule ya Sheria kwa vitendo bila kufuata sheria na utaratibu maalum.
- Chuo cha mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo na Baraza la Wafamasia zilifanya malipo yasiyokuwa na viambatanisho ya kiasi cha shilingi milioni 839.86.

**4.2.9 Mapungufu katika usimamizi wa manunuzi na mikataba**

- Taasisi nne (4) zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi milioni 204.35 nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka.
- Taasisi tisa (9) zilifanya manunuzi yasiyoidhinishwa na bodi ya zabuni ya kiasi cha shilingi milioni 760.89. Hali inaweza kusababisha kutoa zabuni kwa wakandarasi wasio na uwezo.
- Taasisi tatu (3) zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi milioni 144.48. bila ushindanishi. Hii inapelekea kukosekana kwa uwazi na thamani ya fedha katika manunuzi ya umma.
- Taasisi za serikali sita (6) ziliagiza na kulipia huduma na vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 857.88 lakini hazikupokelewa.

**4.2.10 Mapungufu katika usimamizi wa matumizi**

- Taasisi 27 za serikali zilifanya malipo ya jumla ya shilingi bilioni 7.15 ambayo hayana viambatisho vyake. Pia taasisi nne (4) za zilifanya malipo yenye thamani ya shilingi milioni 125.16. Bila kutumia hati za malipo.
- Taasisi kumi na mbili (12) zilifanya malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 4.10 bila kuambatanisha risiti za kielektroniki (EFD) kutoka kwa kila manunuzi waliyoyafanya.
- Taasisi 23 zilifanya malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 1.34 kwa kutumia vifungu visivyostahili bila idhini ya mamlaka. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika bajeti husika.
- Taasisi 21 zimelipa kiasi cha shilingi bilioni 4.96 kwa matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyopitishwa na bila idhini au kibali cha taasisi husika.




- Taasisi nane (8) zilifanya malipo ya shilingi milioni 440.72 zaidi ya kiwango stahiki hupelekea kutofanyika kwa shughuli zingine zenye manufaa kwa umma.

### 4.2.11 Usimamizi wa Mali

- Taasisi nane (8) hazijafanya utaratibu wa kuviondoa vyombo vya moto 380 (Mfano Magari) ambavyo vimefikia ukomo wa kutumika na havina tena thamani ya fedha wala haviwezi kutengenezeka.
- Idara ya Polisi na Wizara ya Elimu ya Ufundi zilinunua mali za kudumu zenye thamani ya shilingi milioni 240.11 ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma hata hivyo mali hizo hazitumiki baada ya kununuliwa.

### 4.2.12 Ukaguzi wa Vyama vya siasa

- Kulikuwa na vyama 21 hadi Juni, 2013 wakati tunakagua hesabu za vyama vya siasa mwaka uliopita. Kati ya vyama 21 ni vyama 12 tu ndivyo

viliwasilisha taarifa za hesabu na vyama tisa (9) havikuwasilisha taarifa za hesabu ambavyo ni UPDP, TADEA, UDP, Demokrasia Makini, CHAUSTA, DP, JAHAZI ASILIA, AFP na CCK.

- Vyama vya siasa sita (6) vilipata hati yenye shaka ambavyo ni CCM, CHADEMA, CUF, NCCR, TLP na CHAUMMA na vyama vya siasa vingine vilipata hati mbaya ambavyo ni NRD, UMD, ADC, APPT, NLD na SAU.
- Kwa mwaka 2013/2014 taarifa za hesabu za vyama vya siasa hazikuwasilishwa kwa wakati kama ilivyopangwa kisheria hivyo kuchelewesha ukaguzi wa vyama vya siasa.

## SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA

Sura hii inatoa muhtasari na majumuisho kuhusu ukaguzi wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) 163 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2014.

## 5.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA

### 5.1.1 Mapungufu katika ukusanyaji na upelekaji wa fedha katika Halmashauri

Sehemu hii inaonyesha mwenendo wa fedha zilizopokelewa na Halmashauri kutoka Serikali Kuu na zilizokusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Jedwali hapa chini linaonyesha makadirio ya fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa na kukusanywa na fedha zisizopokelewa na zisizokusanywa hadi kufikia 30 Juni, 2014.

**Jedwali Na.5: Mchanganuo wa ukusanyaji na upelekaji wa fedha katika Halmashauri**

| Maelezo | Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu( TZS Bilioni) | Fedha za ruzuku ya matumizi ya miradi kutoka Serikali Kuu (TZS Bilioni) | Fedha za makusanyo ya mapato ya ndani (TZS Bilioni) |
|---|---|---|---|
| Makadirio | 2,755.12 | 743.22 | 400.39 |
| Fedha zilizopokelewa/kukusanywa | 2,337.89 | 431.18 | 353.53 |
| Fedha zisizopokelewa/zisizokusanywa | (417.232) | (312,04) | (46.86) |
| Kiasi ambacho hakikupokelewa/kusanywa kwa asilimia | 15.14% | 41.98% | 11.70% |

Mapungufu haya ya kupokea ruzuku na kukusanya mapato pungufu ya makadirio linapelekea kupungua kwa ufanisi wa uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hivyo kupelekea wananchi kukosa huduma muhimu za kijamii na kimaendeleo.

### 5.1.2 Kukosekana kwa ufanisi katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa kihasibu

Tathmini ya ufanisi wa Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha kwa kutumia mfumo wa kihasibu wa 'Epicor Version 9.05' katika Halmashauri 90 umebaini kuwa, licha ya mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa ya ukaguzi ya mwaka jana (2012/2013), bado kuna mapungufu katika mfumo huo ambao hauna muingiliano na viwango vya kimataifa vya kihasibu (IPSAS). Pia usuluhisho wa kihasibu hauwezi kufanywa na kompyuta zilizofungwa katika Halmashauri na hivyo kuwepo haja ya watumishi wa Halmashauri zote kusafiri kwenda Dodoma. Changomoto nyingine ni Halmashauri 27 zilikuwa hazijawekewa mfumo huo wa 'Epicor version 9.05' na hivyo kupelekea kazi nyingi kufanyika nje ya mfumo.

### 5.1.3 Udhaifu katika usimamizi wa mapato ya ndani

**Vitabu vya mapato visivyowasilishwa kwa Ukaguzi**

Vitabu 474 vya stakabadhi za kupokelea mapato kutoka Halmashauri 47 havikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo iliongoza kwa kuwa na vitabu 79, ikifuatiwa na Tunduru vitabu 55 na Wilaya ya Mvomero vitabu 49. Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato ambayo yangeweza kukusanywa au yaliyokusanywa kupitia vitabu hivyo.

**(i) Makusanyo ya mapato ambayo hayakuwasilishwa na Mawakala**

Makusanyo ya mapato kutoka kwa Mawakala yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.91 yatokanayo na vyanzo vya ndani hayakuwasilishwa katika Halmashauri 56 ambapo Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliongoza kwa kuwa na Shilingi bilioni 1.21 ikifuatiwa na Manispaa ya Ilemela Shilingi millioni 886.40. Hii inaweza kusababisha baadhi ya makusanyo hayo kutumika vibaya na Mawakala hivyo kupelekea Halmashauri kushindwa kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo iliyokusudiwa.

**(ii) Mapato ambayo hayajakusanywa na Halmashauri**

Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 54 umebaini kuwa jumla ya kiasi cha Shilingi bilioni 17.12 hakikukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani hivyo kusababisha Halmashauri hizo kutotekeleza majukumu yake ikiwemo shughuli za maendeleo. Halmashauri ya Wilaya ya Mwanza iliongoza kwa kuwa na Shilingi bilioni 1.30 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela Shilingi milioni 845.80. Hali hii ilipelekea baadhi ya halmashauri kushindwa kutekeleza Mipango yake kama zilivyopanga.

**(iii) Mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki**

Makusanyo ya mapato katika Halmashauri 19 yenye thamani ya Shilingi milioni 323 ambayo yalikusanywa na watumishi na watendaji hayakupelekwa benki wala hayakukabidhiwa kwa Halmashauri husika. Kati ya fedha hizo Shilingi milioni 99 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Longido ikifuatiwa na Shilingi milioni 59.3 kutoka Halmashauri ya Wilaya Karatu. Hali hii inaweza kupelekea upotevu wa mapato hayo na hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango ya halmashauri husika.




**(iv) Kiasi cha asilimia 30 ya makusanyo ya kodi ya matumizi ya ardhi kutorudishwa kwenye Halmashauri husika.**

Waraka wa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI unaelekeza kuwa asilimia 30 ya makusanyo ya kodi ya matumizi ya ardhi zitarudishwa kwa Halmashauri husika kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi, ununuzi wa vifaa na zana za upimaji wa ardhi ikiwa ni pamoja na gharama nyingine yoyote inayohusiana na usimamizi wa masuala ya ardhi.

Kinyume na matakwa ya Waraka huo, ilibainika kuwa jumla ya Shilingi bilioni 1.21 sawa na asilimia 30 ya makusanyo yaliyowasilishwa na Halmashauri 32 hayakurudishwa kwa Halmashauri husika kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

### 5.1.4 Udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya fedha

**(i) Malipo yaliyolipwa bila vielelezo**

Malipo ya jumla ya Shilingi bilioni 3.88 yalilipwa katika Halmashauri 80 bila kuwa na vielelezo toshelezi. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba iliongoza ikiwa na malipo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.0 ikifuatiwa na Wilaya ya Longido yenye kiasi cha Shilingi milioni 453.13.

**(ii) Malipo yaliyofanyika bila ya kuwa na hati za malipo**

Halmashauri 20 zilifanya malipo ya jumla ya Shilingi milioni 756.70 bila ya kuwa na hati za malipo. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba iliongoza kwa kuwa na malipo yenye thamani ya Shilingi milioni 250 na kufuatiwa na Halmashauri ya wilaya ya Nyasa kwa kuwa na malipo ya Shilingi milioni 163. Hali hii inapelekea kushindwa kuhakiki uhalali wa malipo husika.

**(iii) Matumizi yaliyofanyika kupitia vifungu tofauti bila kuidhinishwa**

Jumla ya Shilingi bilioni 2.39 katika Halmashauri 47 zililipwa kupitia vifungu tofauti bila kuidhinishwa na Kamati za Fedha. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu iliongoza kwa kuwa na malipo ya Shilingi milioni 393.22 ikifuatiwa na Pangani Shilingi milioni 180.45.

**(iv) Fedha zilizokopwa kutoka akaunti moja kwenda nyingine ndani ya Halmashauri ambazo hazikurejeshwa**

Ukaguzi katika Halmashauri 28 ulibaini kuwa jumla ya Shilingi bilioni 1.81 zilikopwa kutoka akaunti moja kwenda nyingine lakini hazikurejeshwa kwenye akaunti zilipotoka. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliongoza kwa kuwa na kiasi cha Shilingi milioni 359.13 ikifuatiwa na halmashauri ya Wilaya ya Mkalama yenye jumla ya Shilingi milioni 271.48. Hali hii ilisababisha shughuli zilizopangwa katika akaunti husika kutotekelezwa.

**(v) Mishahara ambayo haijarejeshwa Hazina**

Mishahara yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.1 isiyolipwa katika Halmashauri 33 ilikuwa bado haijarejeshwa Hazina. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu iliongoza ikiwa na Shilingi milioni 119.1 ikifuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Sumbawanga lenye Shilingi milioni 89.3.

**(vi) Mishahara iliyolipwa kwa watumishi wasiostahili**

Mishahara ya jumla ya Shilingi bilioni 1.01 ililipwa katika Halmashauri 36 kwa watumishi waliotoroka, waliofariki, waliostaafu na walioachishwa kazi. Hali hii imesababisha upotevu wa fedha za umma hivyo kupelekea Serikali kupata hasara na kushindwa kupeleka huduma muhimu kwa wananchi

**(vii) Makato ya mishahara ambayo hayakuwasilishwa katika taasisi husika**

Mapitio ya Halmashauri 11 kwa mwaka fedha unaoishia 2013/2014 yalionesha jumla ya Shilingi milioni 230.16 ikiwa ni makato ya kisheria kutoka kwa wafanyakazi wa halmashauri hizo hayakupelekwa katika taasisi husika kama LAPF, PSPF, NSSF, PPF na TRA.

**(viii) Ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na Stakabadhi za mfumo wa kielektroniki**

Katika ukaguzi wa Halmashauri 22 ilibainika kwamba, malipo ya stakabadhi ya jumla ya Shilingi bilioni 4.64 hayakuambatanishwa pamoja na stakabadhi zitolewazo na vifaa vya mfumo wa kielektroniki (EFD). Hali hii inatia shaka juu ya kiasi cha Shilingi milioni 834.9 kilichotakiwa kupelekwa kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama kodi. Kwa kutoambatanisha stakabadhi hizo za kielektroni ina maanisha kwamba wale ambao hawatoi stakabadhi hizo wanaashiria ukwepaji wa kodi.

**(ix) Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

Ukaguzi umebaini kuwa katika Halmashauri 15 ambazo zina jukumu la kukusanya kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 2 ya malipo yote ya wasambazaji wa bidhaa na huduma kwa Serikali hazikufanya hivyo. Jumla ya kiasi cha Shilingi milioni 207.59 zilibainika kutokukusanywa na Halmashauri hizo na kupelekwa kwa Kamishna wa Kodi Tanzania hivyo kusababisha Serikali kukosa mapato.

**(x) Malipo yasiyokuwa na manufaa**

Halmashauri tatu zilikuwa na matumizi yasiyokuwa na manufaa ya jumla ya Shilingi milioni 177.18 ambapo jumla ya Shilingi milioni 81.58 zililipwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushindwa kutoza kodi ya ardhi kwa wakati na kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Shilingi milioni 50.59 zililipwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kama fidia kwa uvunjaji wa mkataba. Vile vile, Shilingi milioni 45 zililipwa na Halmashauri ya Mji wa Mpanda kama fidia baada ya kushindwa katika kesi za madai. Hali hii ilisababishwa na Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutozingatia majukumu yao vizuri hasa upande wa usimamizi wa mikataba.

### 5.1.5 Udhaifu katika usimamizi wa mikataba na taratibu za ununuzi

**(i) Ununuzi uliofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni**

Bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 201.38 zilinunuliwa bila kuidhinishwa na Bodi za Zabuni katika Halmashauri 6 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino iliongoza kwa kuwa na ununuzi wa Shilingi milioni 33.15 ikifuatiwa na Wilaya ya Gairo iliyofanya ununuzi wa Shilingi milioni 29.86.Hali hii inaweza kusababisha ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora katika Halmashauri.

**(ii) Fedha zilizolipwa kwa wazabuni wasioidhinishwa**

Shilingi milioni 318.16 zilitumika kununua bidhaa kutoka kwa wazabuni wasio idhinishwa katika Halmashauri kumi na tisa (19). Halmashauri ya Wilaya ya Longido iliongoza kwa kuwa na kiasi cha Shilingi milioni 54 ikifuatiwa Halmashauri ya jiji la Arusha yenye Shilingi milioni 48.14. Hali hii ilipelekea ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora hivyo kuathiri utendaji katika Halmashauri.

**(iii) Ununuzi uliofanyika bila kushindanisha Wazabuni**

Kiasi cha Shilingi milioni 176.92 kililipwa kwa wazabuni katika Halmashauri sita (6) bila kushindanishwa. Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa iliongoza kwa kuwa na ununuzi wa Shilingi milioni 69 ikiwa ni asilimia 39 ya jumla ya ununuzi wote uliofanyika bila kushindanishwa.




**(iv) Bidhaa zilizonunuliwa lakini hazikupokelewa**

Ukaguzi ulibaini kiasi cha Shilingi milioni 156.71 zilizotumika kununua bidhaa ambazo hazikupokelewa katika Halmashauri saba (7). Halmashauri ya Wilaya

ya Iramba iliongoza ikiwa na ununuzi wenye thamani ya Shilingi milioni 62.72 ikiwa ni asilimia 40 ya ununuzi wote uliuofanywa na Halmashauri. Hali hii inaweza kusababisha manunuzi hewa yasiyo na tija kwa Taifa.

**(v) Ununuzi wa vifaa na huduma kwa kutumia masurufu**

Ilibanika kuwa kulikuwa na kiasi cha shilingi milioni 327.24 kilichotolewa na Halmashauri 22 kama masurufu /fedha taslim kwa watumishi mbalimbali kwa ajli ya manunuzi ya bidhaa mbalimbali ambapo ni kinyume na sheria ya ya ununuzi ya mwaka 2011 na kanuni zake za 2013.

## SURA YA SITA

## 6.0 MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA

Ripoti hii inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2014. Ripoti hii inaainisha masuala yanayoathiri ufanisi wa Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma katika kutekeleza na kufikia malengo waliyojiwekea.

## 6.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA

Katika ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma mapungufu mbalimbali yalibainika kama ifuatavyo:

### 6.1.1 Udhaifu katika Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma

#### (i) Utoaji wa Zabuni katika Mazingira ya Kutatanisha

- Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza ilibainika kuwa, Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ilipitisha maamuzi ya kutoa zabuni ya ujenzi wa jengo la Makao makuu ya Mamlaka kwa kampuni ya DF MISTRY ambayo haikupendekezwa na Kamati ya Tathmini ya Zabuni. Kwa mujibu wa ripoti ya tathmini ya zabuni, kampuni iliyopendekezwa kufanya kandarasi hii ilikuwa ni Ngogo Engineering kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.40.

- Pia katika ukaguzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania ilibainika kuwa Mamlaka ilitoa zabuni ya ununuzi wa mfumo wa mawasiliano wa kieletroniki kwa Mkandarasi ambaye hakupendekefzwa na Kamati ya Tathmini ya Zabuni. Kwa mujibu wa ripoti ya tathmini ya zabuni hii, Mkandarasi aliyependekezwa alikuwa ni Web Fountaine kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 6.2. Hata hivyo katika mazingira yasiyoeleweka zabuni hii ilitolewa kwa kampuni ya Phaeros Group BVBA kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 8.37. Kupelekea kulipa Dola za Kimarekani milioni 2.17 zaidi.




**(ii) Mapungufu katika Kutekeleza mipango ya Ununuzi ya Mwaka**

Ukaguzi ulibani kuwa makampuni matatu yalifanya Ununuzi nje ya mpango wa Ununuzi wa mwaka ambapo ni kinyume na Kanuni Na.69(1) (b) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa umma za mwaka 2013. Makampuni hayo ni Kampuni ya Simu Tanzania kiasi cha Shilingi bilioni 45.7, Benki Kuu ya Tanzania kiasi cha Shilingi Bilioni 12.41 na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza kiasi cha Shilingi milioni 151.74.

**(iii) Ununuzi wa Bidhaa na Huduma bila Ushindani**

Ukaguzi wa nyaraka mbali mbali za ununuzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibaini ununuzi wa bidhaa na huduma bila ushindani. Kasoro hii ilibainika katika ukaguzi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC) ambapo kiasi cha Shilingi milioni 219.87 zilitumika kununua bidhaa bila ushindani, na Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara Moshi kilitumia kiasi cha Shilingi milioni 335.9 katika ununuzi wa bidhaa na huduma bila ushindani. Ununuzi huu ulizuia fursa ya kupata bidhaa kwa bei nafuu na ubora stahiki.

**(iv) Utoaji Zabuni kwa Wakandarasi bila Kuzingatia Uthibitisho wa Ulipaji Kodi**

Ukaguzi wa mikataba 10 yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.40 iliyoingiwa kati ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza na wakandariasi haikuwa na vyeti vya kuthibitisha ulipaji wa kodi, hivyo kutothibitika juu ya malipo ya kodi yaliotakiwa kulipwa na Wakandarasi husika katika Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**(v) Kutokamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la 'Linear Accelerator Treatment' katika Taasisi ya Kansa Ocean Road**

Ukaguzi ulibaini kutokamilika kwa mradi wa ujenzi wa jengo la *'Linear Accelerator Treatment'* kulikopelekea lengo lililokusudiwa la kutoa huduma kwa wagonjwa wa kansa nchini kutotimizwa ipasavyo. Ujenzi huo ulitakiwa kumalizika ndani ya wiki 32 yaani hadi Julai 2014, hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014 ujenzi huu ulikuwa bado haujakamilika kutokana na Serikali kuchelewa kutoa fedha za mradi.

### 6.1.2 Matumizi yasiyo sahihi ya Rasilimali za Umma

**(i) Kasoro zilizobainika katika Usimamizi wa Mafuta ya Magari**

Ukaguzi ulibaini uwepo wa kasoro kadhaa kwenye usimamizi wa mafuta ya magari katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma tisa(9).Baadhi ya kasoro hizo ni kama ifuatavyo.

- Kutofanyika kwa usuluhishi baina ya kuponi za kuchukulia mafuta, Ankara na hati za kupokelea bidhaa.
- Vitabu vya kusaini vya magari havikuhakikiwa na maafisa waandamizi.
- Baadhi ya Vitabu havikuwa na taarifa za kutosheleza na baadhi ya vitabu havikuwepo kabisa.
- Kutofautiana kwa taarifa kati ya taarifa ya mwezi ya matumizi ya mafuta na vitabu vya kusainia magari.

Hali hiyo inaongeza mzigo wa uendeshaji na hasara kwa Mashirika hayo na Serikali kwa ujumla.

**(ii) Vifo vya Wanyama pori Kutokana na Ajali za Barabarani**

Mbuga ya wanyama ya Mikumi iliyo chini ya Shirika la Hifadhi ya Wanyama Pori la Taifa (TANAPA) imebainika kuwa na tatizo la kuuwawa kwa wanyama katika mbuga hiyo kutokana na ajali za barabarani. Kulingana na ripoti ya usimamizi wa viumbe hai, jumla ya wanyama pori 107 waliripotiwa kugongwa na kufa katika ajali za barabarani kati ya kipindi cha Julai 2013 hadi mwezi Machi 2014.

**(iii) Tofauti kati ya Deni la Mfuko wa Huduma za Mawasiliano Bara na Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar**

Ukaguzi uliofanywa katika Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulibaini tofauti ya deni lililoripotiwa baina ya Mfuko na Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar. Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar ilikiri kudaiwa kiasi cha shilingi milioni 135.67 dhidi ya deni halisi la Shilingi bilioni 1.27, ilipelekea kuwa na tofauti kubwa ya kiasi cha Shilingi bilioni

1.14 baina ya taarifa za Taasisi hizi mbili na hivyo kutoa viashiria vya uwepo wa mgogoro endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kuondoa tofauti iliyopo.

### 6.1.3 Hali ya Madeni ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Ukaguzi ulibaini kuendelea kukua kwa deni la serikali, hadi sasa limefikia kiasi cha Shilingi trilioni 1.88 hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2014. Madeni haya yanajumuisha mikopo iliyokopeshwa Serikali moja kwa moja, kwa Mashirika ya Umma/Taasisi za Serikali kwa dhamana ya Serikali na michango ya wanachama ambayo haijalipwa. Kiasi hiki hakijumuishi Shilingi trilioni 7.1 ambazo Serikali inadaiwa na PSPF tangu mwaka 1999 kwa kuwalipa mafao wastaafu ambao hawakuwa wakichangia. Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa baadhi ya madeni haya hayalipwi kabisa na mengine yanalipwa kwa kasi ndogo sana na hayana mikataba ya mikopo wala dhamana ya Serikali.




### 6.1.4 Masuala yahusuyo Utawala Bora

Utawala bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu, usawa na kufuata utawala wa sheria. Wakati wa ukaguzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, nilibaini kuwepo kwa masuala kadhaa ambayo ni kinyume na kanuni na taratibu za utawala bora kama ifuatavyo:

**(i) Shirika la Masoko Kariakoo**

Ilibainika kuwa Shirika hili limekuwa likiendeshwa bila chombo halali cha usimamizi tangu mwaka 2000 baada ya kuvunjwa kwa iliyokuwa Bodi ya Wakurugenzi na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kutokana na kuvunjwa kwa Bodi ya Wakurugenzi, uendeshaji wa Shirika hilo uliwekwa chini ya Jiji la Dar es Salaam ambalo liliteua Baraza la Uendeshaji kama chombo cha uangalizi wa Shirika kinyume na Sheria ya Masoko ya Kariakoo. Zaidi ya hayo, Mkurugenzi Mkuu ambaye alitakiwa kuteuliwa na Rais aliteuliwa na Waziri kinyume na sheria.

Ukiukwaji huo wa Sheria ya uanzishwaji wa Shirika kunafanya uwepo wa Baraza hilo la uendeshaji kutokuwa halali na hivyo maamuzi yote yaliyofanywa katika kipindi hicho kuwa kinyume cha Sheria.

**(ii) Kutoteuliwa kwa Wakati kwa Bodi za Wakurugenzi**

Wakati wa ukaguzi wa masuala ya utawala bora katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ilibainika kuwa muda wa Bodi kadhaa ulikuwa umekwisha pasipo kuwa na hatua za kuteua Bodi mpya.

Hadi wakati wa kuandaa ripoti hii Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kumi na sita (16) Bodi zake zilikuwa zimekwisha muda wake. Mashirika hayo ni Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFIRI), Chuo cha Mipango (IRDP), Bodi ya Katani Tanzania, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Bodi ya Pareto Tanzania, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC), Makumbusho ya Taifa, Kamisheni ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi (NLUPC), Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) na Shirika la Masoko Kariakoo.

Hali hii inaathiri ufanisi wa mashirika hayo katika kutimiza majukumu yake.

## SURA YA SABA

## MUHTASARI WA RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

### 7.0 UTANGULIZI

Sura hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo lengo kuu la fedha hizo za miradi ni kutumika katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ili kukuza uchumi wa nchi na kutoa huduma muhimu za kijamii.

Ukaguzi wa miradi katika kipindi hiki ulihusisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Maendeleo ya Afya (HBF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP), Mfuko wa barabara(RF) na miradi mingine inayofadhiliwa na wahisani mbalimbali ndani na nje ya nchi.

### 7.1 MATOKEO YA UKAGUZI

#### 7.1.1 Tathmini ya fedha za Miradi ya Maendeleo

Katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo, jumla ya fedha zilizokuwepo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni Shilingi trilioni 3.59 ikijumuisha fedha za bakaa Shilingi bilioni 560.91 na fedha zilizopokelewa shilingi trilioni 3.03. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2014 kulikuwa na kiasi kisichotumika cha Shilingi bilioni 495.92 sawa na asilimia 14 ikimanisha kuwa fedha zilizotumika ni Shilingi trilioni 3.09 sawa na asilimia 86 kama inavyoonekana katika jedwali Na. 6:

**Jedwali Na. 6: Tathmini ya fedha za Miradi ya Maendeleo**

| Miradi (Sh. milioni) | Fedha ambazo hazikutumika kipindi kilichopita | Fedha iliyopokelewa | Kiasi kilichokuwepo kwa ajili ya utekelezaji | Matumizi | Kiasi ambacho hakikutumika | Bakaa katika % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ASDP | 17,986 | 60,788 | 78,774 | 50,352 | 28,421 | 36.08 |
| HBF | 25,970 | 86,137 | 112,106 | 89,102 | 23,004 | 20.52 |
| RF | 34,507 | 152,444 | 186,951 | 142,254 | 44,698 | 23.91 |
| TASAF | 2,149 | 14,092 | 16,241 | 14,335 | 1,906 | 11.74 |
| WSDP | 80,288 | 184,029 | 264,317 | 194,818 | 69,499 | 26.29 |
| **Jumla Ndogo** | **160,899** | **497,490** | **658,389** | **490,862** | **167,527** | 25.44 |
| Miradi Mingine | 400,008 | 2,527,664 | 2,927,673 | 2,599,283 | 328,389 | 11.22 |
| **Jumla Kuu** | **560,907** | **3,025,154** | **3,586,062** | **3,090,145** | **495,916** | 13.83 |

Jumla ya fedha ambazo hazikutumika kwa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha ni asilimia 13.83 ya fedha yote iliyokuwepo. Uchambuzi unaonyesha asilimia 25.44 ya fedha zilizokuwepo hazikuweza kutumika katika miradi mikubwa mitano hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha.

Pia katika miradi mingine asilimia 11.22 ya fedha zilizokuwepo hazikuweza kutumika. Kiasi kikubwa cha bakaa kimetokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi, utaratibu mrefu wa manunuzi na udhaifu wa utekelezaji wa miradi katika halmashauri. Na kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii fedha za matumizi ya miezi sita inayofuata ilitolewa mwishoni mwa mwaka.

**Mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:**

### 7.1.2 Masuala ya Usimamizi wa Bajeti

#### (i) Matumizi Yaliyofanywa kwa Kutumia Vifungu Visivyohusika

Matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 1.32 yalilipwa kwa kutumia vifungu visivyohusika na halmashauri sabini na nane (78). Mradi wa ASDP ulijumuisha Halmashauri 13 zenye jumla ya shilingi milioni 106.21. Mradi wa HBF ulijumuisha Halmashauri 33 zenye jumla ya shilingi milioni 479.42. Mradi wa Barabara ulijumuisha Halmashauri 13 zenye jumla ya shilingi milioni 285.07. Mradi wa Maji ulijumuisha Halmashauri 19 zenye jumla ya shilingi milioni 445.56. Matumizi yaliyofanywa nje ya vifungu vilivyoidhinishwa yanaathiri utekelezaji wa shughuli za miradi iliyopangwa.

#### (ii) Matumizi Yaliyofanywa Nje ya Bajeti Iliyoidhinishwa.

Halmashauri thelathini na nne (34) zilifanya matumizi ya trilioni 1.45 nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamikia shughuli mbalimbali, ambapo Mradi wa ASDP ilijumuisha Halmashauri 4 zenye jumla ya shilingi milioni 63.25, Mradi wa RF ilijumuisha Halmashauri 27 zenye jumla ya shilingi milioni 988 na Miradi mingine mitatu (3) yenye jumla ya shilingi milioni 398.26. Hii ina maana kuwa baadhi ya kazi zilizoainishwa kwenye mpango kazi ulioidhinishwa hazikutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

#### (iii) Upungufu wa Fedha za Ruzuku.

Baadhi ya halmashauri hazikutekeleza shughuli zilizokuwa zimepangwa kutokana na upungufu wa fedha za ruzuku ambazo hazikutolewa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa. kiasi cha Shilingi bilioni 52.69 hakikupokelewa kama ilivyoidhinishwa kwenye bajeti, ambapo Miradi ya ASDP ilijumuisha Halmashauri 85 zenye jumla ya shilingi bilioni 34.54, RF ilijumuisha Halmashauri 72 zenye jumla ya shilingi bilioni 11.75, TASAF ilijumuisha Halmashauri moja yenye jumla ya shilingi milioni 245.20 na Miradi mingine minne (4) yenye jumla ya shilingi bilioni 6.15. Hali hii inaweza kusababisha serikali kutofikia malengo iliyojiwekea.

#### (iv) Ucheleweshwaji wa Uhamishaji wa Fedha.

Halmashauri ishirini na tatu (23) zilichelewa sana kupokea kiasi cha Shilingi bilioni 12.04 kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mfuko wa Afya. Kulikuwa na ucheleweshaji wa takribani miezi mitano ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli za miradi kwa wakati.




**(v) Miradi ambayo haikutekelezwa**

Jumla ya miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni 44.17 haikutekelezwa kutokana na kukosekana kwa fedha za miradi; ambapo Mfuko wa Afya ulijumuisha Halmashauri 41 zenye miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 4.00; na miradi mingine mitano (5) yenye thamani ya bilioni 40.70

### 7.1.3 Mapungufu katika usimamizi wa fedha

**(i) Malipo yenye nyaraka pungufu.**

Malipo yenye nyaraka pungufu yenye thamani ya shilingi bilioni 6.51 yalifanyika kwa Halmashauri mia moja na thelathini na nane (138) ambapo mradi wa ASDP ulijumuisha Halmashauri 23 zenye jumla ya Shilingi milioni 688.59, HBF Halmashauri 47 zenye kiasi cha shilingi milioni 689.83,WSDP Halmashauri 30 zenye jumla ya Shilingi bilioni 1.22, Mfuko wa Barabara Halmashauri 23 zenye jumla ya Shilingi milioni 340.19 ,TASAF Halmashauri 3 zenye jumla ya shilingi milioni 32.57 hivyo uhalali na usahihi wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

**(ii) Malipo yaliyofanyika bila hati za malipo.**

Matumizi ya jumla ya Shilingi milioni 465.02 yalibainika kufanyika bila kuwepo hati za malipo. Katika matumizi hayo, mradi wa ASDP ulijumuisha Halmashauri 9 zenye jumla ya Shilingi milioni 28.61 , HBF Halmashauri 14 zenye kiasi cha Shilingi milioni 194.43 , RF Halmashauri 11 zenye kiasi cha Shilingi 111.42, na WSDP Halmashauri 6 zenye kiasi cha Shilingi milioni 130.54 hivyo kupelekea uhalali wa malipo hayo kushindwa kuthibitika.

**(iii) Matumizi ya Fedha za Bakaa bila Idhini Kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.**

Halmashauri (14) zilitumia fedha za bakaa za Mfuko wa barabara kiasi cha Shilingi bilioni 2.03 bila kupata kibali toka Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI kinyume na Aya 3.5 ya makubaliano ya mwaka ya utekelezaji wa kazi za barabara Wilayani, Mijini na Mitaani. Kukosekana kwa idhini hiyo, fedha zilizobaki mwaka 2012/13 hazikuwa kwenye makubaliano ya utekelezaji wa

kazi za barabara kwa mwaka 2013/14 na kuna uwezekano fedha hiyo ilitumika kugharamia shughuli ambazo hazikukusudiwa.

**(iv) Manunuzi ya Bidhaa na Huduma bila Kudai Stakabadhi ya Fedha ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).**

Miradi minne (4) ilinunua bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila ya kudai stakabadhi ya fedha ya Mamlaka ya Mapato Tanzania,ambapo Mradi wa Kuboresha Miji Tanzania-(TSCP- TAMISEMI) shilingi milioni 11.33, Mradi Shirikishi Katika Usimamizi wa Misitu (PFM) – TAMISEMI shilingi milini 8.47, Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Mkoa wa Dar-es-salaam(DART) shilingi milioni 59.41, Programu ya Uimarishaji wa Miji Serikali za Mitaa (ULGSP) shilingi milioni 571.45.

### 7.1.4 Masuala Yanayohusu Ununuzi na Usimamizi wa Mikataba.

**(i) Ununuzi wa Vifaa na Huduma usioidhinishwa na Bodi ya Zabuni.**

Ilibainika kuwa Halmashauri ishirini na sita (26) zimefanya ununuzi wa mali, vifaa na huduma vya thamani ya Shilingi bilioni 2.01 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila idhini ya Bodi ya Wazabuni. Mradi wa ASDP ilijumuisha Halmashauri 3 zenye thamani ya shilling milioni 82.53,HBF Halmashauri 9 yenye thamani ya shillingi milioni 441.25, RF Halmashauri 14 ilikuwa na thamani ya shillingi bilioni 1.49. Hali hii inaweza kupelekea ununuzi huo kufanyika nje ya mpango wa mwaka wa ununuzi hivyo kuathiri makadirio ambayo tayari yaliidhinishwa na Halmashauri husika.

**(ii) Ununuzi uliofanywa bila kushindanisha Wazabuni.**

Jumla ya shilingi milioni 592.22 zilitumika kufanya ununuzi katika Halmashauri 15 bila kushindanisha wazabuni katika miradi ya maendeleo ambapo mradi wa ASDP ulikuwa na ununuzi wa Shilingi milioni 42.73, HBF shilingi milioni 549.49 .Hali hii inaweza kupelekea ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

**(iii) Ununuzi wa Huduma toka kwa Wauzaji Wasioidhinishwa.**

Halmashauri ishirini na tano (25) zilifanya ununuzi wa mali, kazi za ujenzi na zisizo za ushauri za Shilingi milioni 457.95 kutoka kwa wauzaji ambao hawakuthibitishwa na wakala wa ununuzi wa Serikali (GPSA) na Bodi za Zabuni katika ununuzi huo; ambapo mradi wa ASDP ulijumuisha Halmashauri 6 zenye thamani ya shilingi milioni 119.61 na HBF halmashauri 19 zenye thamani ya shilingi milioni 338.34.

**(iv) Mali na Vifaa vilivyolipiwa lakini havikupokelewa.**

Mali na Vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 594.36 vilinunuliwa na watekelezaji wa miradi mbalimbali lakini havikupokelewa. Katika manunuzi hayo mradi wa Afya (HBF) ulijumuisha Halmashauri 11 zenye jumla ya shilingi milioni 322.89 na miradi wa Maji (WSDP) ilijumisha

watekelezaji watano (5) wenye jumla ya shilingi milioni 271.47. Kutopokelewa kunaashiria kutokufanyika kwa manunuzi ya bidhaa hizo na kunazorotesha utekelezaji wa miradi hiyo.




**(v) Ununuzi uliofanyika bila kibali cha Bohari Kuu.**

Kiasi cha Shilingi bilioni 1.12 kililipwa na Halmashauri thelathini (33) ikiwa ni ununuzi wa dawa na vifaa vya tiba kwa wazabuni binafsi kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Afya (HBF) bila kibali cha Bohari Kuu ya Dawa. Hali hii inaadhiri upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa bei ya chini na zinazokidhi ubora unaotakiwa.

**(vi) Tozo za Kutotimiza Masharti ya Mkataba.**

Halmashauri kumi na nane (18) ziliingia mikataba na Wakandarasi mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara. Muda wa mkataba uliainishwa kwenye masharti maalum ya mkataba ulibainika kumalizika na hakuna nyongeza ya muda wa mkataba uliotolewa kwa Wakandarasi. Hata hivyo, Wakandarasi waliochelewa kumaliza kazi, muda huokuongezwa na hawakutozwa tozo ya kiasi cha Shilingi milioni 340.58 kama ilivyoanishwa kwenye mikataba yao. Kutokamilika kwa kazi kwa muda uliopangwa kunasababisha kuongezeka kwa gharama za mradi.

**(vii) Kodi ya zuio kwa Malipo ya Wakandarasi haikupelekwa Mamlaka ya Mapato.**

Kodi ya zuio yenye thamani ya shilingi bilioni 2.36 inayotakiwa kukusanywa kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na makusanyo hayo

yawasilishwe kwa Mamlaka ya Mapato ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi. Mapitio ya malipo yaliyofanyika ndani ya mwaka wa fedha kwa Wakandarasi umeonyesha kuwa mfuko wa barabara ulijumuisha Halmashauri ishirini na tatu (23) zenye thamani ya shilingi milioni 817.34 na miradi mingine mitatu (3) yenye thamani ya shilingi bilioni 1.54 hazikupelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**(viii) Tozo ya Riba kwa Kuchelewa Kulipa Madai kwa wakandarasi.**

Kiasi cha Shilingi bilioni 3.52 kililipwa kama tozo ya riba kutoka kwenye miradi mitatu (3) kwa sababu ya kuchelewesha malipo ya hati za madai kwa Wakandarasi ambapo Mradi wa Kusaidia Sekta ya Barabara (RSSP1) ulikuwa na jumla ya shilingi milioni 768.90; Singida - Babati - Minjingu - Mradi wa Barabara shilingi bilioni 2.54 na Mradi wa Kusaidia Sekta ya Barabara –DANIDA shilingi milioni 207.61. Serikali inashauriwa kupeleka fedha za kutosha na kwa wakati ili kuzuia tozo ya riba.

## SURA YA NANE

## 8.0 MUHTASARI WA RIPOTI ZA KAGUZI MAALUM

Sura hii inatoa muhtasari na majumuisho kuhusu kaguzi maalum zilizofanyika katika Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2014.

## 8.1 MATOKEO YA UKAGUZI MAALUM

### 8.1.1 Masuala yatokanayo na ukaguzi maalum wa Serikali Kuu

Mwaka 2013/2014 kulikuwa na kaguzi maalum nane (8) ambazo zilibaini masuala yafuatayo:

**(i) Mfumo mzima wa ununuzi na usambazaji wa pembejeo za kilimo katika sekta ya kilimo cha tumbaku chini ya Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku kanda ya Magharibi (WETCU) - Tabora kwa miaka ya fedha 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013**

Baadhi ya masuala yaliyobainika katika ukaguzi huu ni pamoja na masuala yafutatayo:

- Utaratibu wa kuwapata Wazabuni wa usafirishaji haukuwa wa ushindani na wala haukuwa wazi. Pia wazabuni walipewa zabuni bila kuwasilisha nyaraka za kuombea zabuni na bila kupitishwa na Bodi ya Zabuni.
- Hapakuwa na utunzaji unaoridhisha wa kumbukumbu na taarifa zenye kuwezesha kujua idadi ya miche iliyohitajika kwa kila Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS).
- Maelekezo ya malipo mengi yaliyofanyika benki yalitolewa na Meneja Uendeshaji wa WETCU ambaye hakuwa mwidhinishaji wa malipo na pia bila uongozi wa WETCU na vyama vya msingi (AMCOS) kuwa na taarifa.

**(ii) Ujenzi wa jengo la kumbi za watu mashuhuri katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere uliopo Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 hadi 2011/2012**

Ukaguzi huu maalumu ulibaini masuala mbalimbali pamoja na ya yafuatayo:

- Kutopatikana kwa mkataba, nyaraka na vielelezo kwenye majalada ya ofisi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) na yale ya Kiwanja cha kimataifa cha Mwl. J. K . Nyerere (JNIA) zinazoonyesha gharama halisi za ujenzi wa jengo. Hii ni kutokana na kwamba mkandarasi na mfadhili wa mradi hawakukabidhi nyaraka za ujenzi Serikalini na hivyo kushindwa kufahamu gharama halisi iliyolipwa na Mfadhili huyo.

**(iii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu matatizo yanayozikumba Balozi za Tanzania uliofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 mpaka 2012/2013**

Ukaguzi huu maalumu ulibaini ulibaini masuala mbalimbali pamoja na ya yafuatayo:

- Makisio ya matumizi yamekuwa yakiandaliwa bila kuzingatia mahitaji halisi ya Balozi. Matokeo yake balozi zimekuwa haziwezi kulipia huduma zote muhimu na hivyo kuwa na madeni na hata hukatiwa baadhi ya huduma muhimu kama vile umeme.
- Makusanyo ya mapato yamekuwa hayaridhishi kutokana na kukosekana kwa mikakati balozini ya kuitangaza nchi ya Tanzania.
- Fedha ya maendeleo imekua haitengwi ili kuendeleza viwanja balozini na pia kukarabati majengo.
- Watumishi walioko ubalozini kutorejea nchini baada ya muda wao wa utumishi kukoma au baada ya kustaafu. Watumishi hao wameendelea kulipwa posho ya huduma bila ya kuwa na mkataba.

**(iv) Utekelezaji wa mikataba ya ujenzi wa mradi wa usambazaji maji Chalinze – Awamu ya pili**

**Ukaguzi huu maalumu ulibaini yafuatayo:**

- Kutokuwa na usimamizi wa kutosha wa mikataba na hivyo kupelekea mradi kuchelewa kukamilika kati ya miezi kumi na nane (18) hadi miezi thelasini na sita (36) na kusababisha kusitishwa kwa mikataba.
- Ukaguzi wa taarifa za usanifu na michoro iliyotayarishwa na Mhandisi Mshauri ulibaini kuwa kazi ilikuwa imefanyika chini ya kiwango na hivyo kupelekea kuwa na marekebisho mengi yaliyosababisha nyongeza za mkataba wa awali na kupelekea ongezeko la mara kwa mara la gharama ya mkataba.
- Hati za madai za Wakandarasi zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 5.26 (sawa na Shilingi bilioni 6.83) zililipwa ingawa zilikuwa hazionyeshi uchambuzi wa gharama kwa kuoanisha kazi zilizofanyika kwa kufuata mchanganuo wa gharama za ujenzi (BOQ).
- Mkandarasi Mshauri aliwasilisha makadirio ya riba ya kiasi cha Shilingi bilioni 3.90 (sawa na dola za kimarekani milioni 2.8) kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi kwa zaidi ya siku 307.

**(v) Fedha zilizotumiwa na wizara mbalimbali kuchapisha hotuba baada ya kuidhinishwa na bunge la bajeti kwa miaka ya 2011/2012 na 2012/2013**

Ukaguzi huu maalumu ulibaini ulibaini masuala mbalimbali pamoja na ya yafuatayo:

- Ukosefu wa sheria zinazosimamia uchapishaji wa bajeti katika magazeti.
- Kukosekana kwa mwongozo wala waraka unaotoa ukomo wa matangazo kuhusu wakati gani, mara ngapi bajeti itangazwe, vyombo vingapi vya matangazo vitumike na kiasi gani kitumike.

**(vi) Wizara ya Ujenzi kuhusu uhalali wa fedha shilingi bilioni 252.98 za ujenzi wa miradi maalum ya barabara.**

Ukaguzi huu maalumu ulibaini ulibaini masuala mbalimbali pamoja na ya yafuatayo:

- Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilibadilisha matumizi ya fedha zilizopelekwa kutoka Wizara ya Ujenzi bila kuijulisha wizara na pia nyaraka zilizotumika kufanya mabadiliko hayo kutowasilishwa kwa ajili ya mapitio.
- Shilingi bilioni 175.23 zilihamishwa kwenda akaunti ya maendeleo ya Wakala wa Bararbara Tanzania (TANROADS). Hata hivyo, kati ya kiasi hicho TANROADS ilifanya matumizi ya shilingi bilioni 3.05 ambacho maelezo na nyaraka hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.
- Kiasi cha shilingi bilioni 13.39 zilitumika katika matengenezo ya barabara za wilaya ambazo hupokea mgao wa fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara.
- Shilingi bilioni 6.60 zilionyeshwa kwenye taarifa ya madeni yaliyowasilishwa Wizara ya Ujenzi na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), lakini madeni hayo yalikuwa yamelipwa na ofisi za mkoa za Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)

**(vii) Taarifa ya fedha zilizotumika katika mkutano wa kimataifa SMART Partnership Dialogue wa mwaka 2013 uliofanyika kuanzia mwezi Julai, 2012 hadi Januari, 2014**

**Ukaguzi huu maalumu ulibaini ulibaini masuala mbalimbali pamoja na ya yafuatayo:**

- Malipo ya shilingi milioni 187.45 yalifanywa kwa Kampuni ya Simply Computers Tanzania Ltd kwa ajili ya manunuzi ya vifaa vya mkutano. Hata hivyo vifaa vilipokelewa baada ya kukamilika kwa mkutano huo.
- Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya tiketi za usafiri wa ndege ilikuwa shilingi milioni 21 lakini kiasi halisi kilichotumika kwa tiketi za ndege ni shilingi milioni 187. Hii ilipelekea kuwepo matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwa shilingi milioni 166.

**(viii) Mradi wa manunuzi ya matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2014**

**Ukaguzi huu maalumu ulibaini ulibaini masuala mbalimbali pamoja na ya yafuatayo:**

- Mzabuni ESCORT LTD alishinda zabuni ya kusambaza matrekta, mashine za kusukumia maji, zana za kilimo na huduma nyingine kwa gharama ya dola za marekani milioni 40. Mzabuni huyu aliomba zabuni kwa dola za Kimarekani milioni 35.53 na kusababisha tofauti ya malipo ya dola za Kimarekani milioni 4.48 bila maelezo ya kutosheleza.




- Ununuzi wa matrekta 2,114 pamoja na zana za kilimo 4,450 yalifanyika bila ya kufuata sheria na kanuni za ununuzi wa umma.
- Ukosefu wa eneo maalum au ghala kwa ajili ya kuhifadhia matrekta na zana za kilimo hivyo kupelekea uharibifu wa zana za kilimo kutokana na mvua na jua. Pia mashine za umwagiliaji 31 zenye thamani ya Shilingi milioni 177.18 ziliungua moto kutokana na utunzaji usio makini.
- Ukaguzi ulibaini uwepo wa hasara ya Shilingi milioni 261.03 iliyotokana na kunyofolewa vipuri kwenye matrekta matano na zana za kilimo (Power tillers) 16.
- Afisa Masuuli hakuteua kamati ya mapokezi na kukubali vifaa hivyo kupelekea kupokelewa kwa vifaa visivyokuwa na viwango vyenye thamani ya dola za kimarekani 88,728 (sawa na Shilingi milioni 149.51) vilivyoletwa na Mzabuni ESCORT Company.

- Kutokukusanywa kwa mapato ya Shilingi bilioni 6.68 yanayotokana na mauzo ya matrekta na zana za kilimo kwa mkopo kwa wateja 117. Mapato hayo yalikuwa hayajakusanywa kwa zaidi ya miaka matatu bila maelezo yanayojitosheleza.
- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilipokea Shilingi bilioni 5.17 kutoka Hazina kwa ajili ya mradi wa matrekta na zana za kilimo wa SUMA JKT. Nyaraka za matumizi ya Shilingi milioni 498.92 hazikuwasilishwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya ukaguzi.

**8.1.2 Masuala yatokanayo na ukaguzi maalum wa Serikali za Mitaa**

**(i) Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga:**

**Ukaguzi maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ulikuwa ni wa mwaka wa fedha 2011/2012. Baadhi ya masuala yaliyojitokeza ni kama yafuatayo:**

- Kiasi cha Shilingi bilioni 1.1 kilitumika katika kutekeleza shughuli za miaka ya nyuma za Mfuko wa Barabara bila ya kupata idhini kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.
- Mafuta yaliyonunuliwa yenye thamani ya shilingi milioni 272.93 hayakuweza kuthibitishwa jinsi yalivyotumika kwa sababu kumbukumbu za mwisho za matumizi hazikuweza kupatikana.
- Hati za malipo za jumla ya Shilingi milioni 288.35 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hii inamaanisha kwamba usahihi na uhalali wa matumizi yaliyofanywa haukuweza kuthibitishwa.

**(ii) Halmashauri ya Manispaa ya Ilala**

**Ukaguzi maalumu ulibaini masuala mbalimbali pamoja na yafuatayo:**

- Mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye Ushuru wa Huduma “Service Levy” ya jumla ya Shilingi milioni 8.12 hayakuingizwa kwenye daftari la kukusanyia mapato.
- Kutokusanywa kwa mapato yanayotokana na mabango kiasi cha Shilingi milioni 235.87 kwa mwaka wa fedha 2011/12 na 2012/13.
- Ucheleweshaji katika kuidhinisha vibali vya ujenzi ambao huwa unafanywa na Madiwani uliopelekea kushindwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni 52.65

**(iii) Halmashauri ya Manispaa ya kinondoni**

Ukaguzi maalumu ulibaini mbalimbali pamoja na yafuatayo:

- Kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha wa mikataba ya uwekezaji ambayo imesababisha majengo kujengwa kinyume na matakwa ya mkataba. Hali hii ilitokea kutokana na kutokuwepo kwa msimamizi upande wa Halmashauri katika kipindi chote cha utekelezaji wa miradi.

- Halmashauri haina uwezo wa kutosha katika kusimamia masuala ya uwekezaji. Kwa sasa, masuala ya uwekezaji yanasimamiwa na Mtathmini wa Manispaa bila kuwahusisha watumishi wengine wa Halmashauri kwa kuwa hawana weledi katika eneo hili.
- Halmashauri iliingia mkataba na wapangaji katika nyumba za Magomeni "Magomeni Quarters". Hata hivyo, mapitio ya makubaliano ya mkataba yalibaini kulikuwa na mapungufu katika mkataba uliosainiwa na kupelekea Halmashauri kupata hasara ya kiasi cha Shilingi milioni 736.32 zilizolipwa kwa wapangaji husika kitu ambacho hakikuwepo kwenye mkataba

**(iv) Halmashauri ya Jiji la Mwanza**

Ufuatao ni muhtasari wa baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalumu katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza:

- Makusanyo ya mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 3.08 kwa mwaka wa fedha 2010/11 na 2011/12 hayakuweza kuthibitika kuwasilishwa kwenye Halmashauri na Mawakala wa makusanyo ya mapato.
- Kutokulipa mkopo wa Shilingi milioni 856.89 (Mtaji na riba) kwa benki ya CRDB licha ya ukweli kwamba muda wa mkataba ulikuwa umemalizika.
- Halmashauri ilifanya matumizi ya jumla ya shilingi milioni 863.02 kwa ununuzi wa mafuta nje ya bajeti bila ya kuidhinishwa na Kamati ya Fedha.
- Hati za malipo ya jumla ya Shilingi bilioni 1.44 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wakati zilipohitajika kwa hivyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitika.

**(v) Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi**

Ufuatao ni muhtasari wa baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi:

- Kulikuwa na malipo yenye udanganyifu ya posho za kujikimu pamoja na posho za masaa ya ziada ya jumla ya Shilingi Milioni 113.43 kwa watumishi wa Halmashauri kutokana na kuingiliana kwa tarehe katika kufanya shughuli mbili tofauti.
- Makusanyo ya mapato ya Shilingi milioni 43.16 kwa mwaka wa fedha 2012/13 na 2013/14 hayakuwasilishwa Halmashauri na mawakala wa kukusanya ushuru.
- Hati za malipo za jumla ya Shilingi milioni 317.94 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wakati zilipo hitajika. Hii inamaanisha kuwa uhalali wa malipo haya haukuweza kuthibitishwa.

**(vi) Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi**

Matokeo ya ukaguzi maalumu kwa muhutasari yalikuwa kama ifuatavyo:

- Halmashauri ilipata hasara ya Shilingi milioni 37.99 kutokana na kutotumia bei zilizoidhinishwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini 'GPSA'
- Kukosekana kwa hati za malipo ya jumla ya Shilingi bilioni 1.81 kwa ajili ya ukaguzi kulikopelekea kutokudhibitishwa kwa uhalali wa malipo hayo.
- Kiasi cha shilingi milioni 108.43 kilitumiwa na Halmashauri kununulia pikipiki 42 na gari moja kwa ajili ya madiwani katika utaratibu wa mikopo kinyume na agizo namba 41(6) la memoranda ya fedha za Halmashauri ya Mwaka 2009. Hadi wakati wa ukaguzi (Octoba 2013), hapakuwepo na dalili zozote za kurejesha mikopo hiyo kutoka kwa madiwani.
- Katika mwaka wa fedha 2010/11, jumla ya Shilingi Milioni 375.53. zilitumika katika ujenzi wa bwawa. Hata hivyo, ripoti ya ukaguzi kwa kazi zilizofanyika ya tarehe 14 Februari, 2011 ilitoa mapungufu mbalimbali ambapo ilionekana kwamba bwawa halikuwa na uwezo wa kuhifadhi maji. Kwa hali hiyo, Halmashauri haikupata thamani ya fedha kwa matumizi ambayo yalikuwa yameshafanyika.

### 8.1.3 Masuala yatokanayo na ukaguzi maalum wa Mashirika ya Umma

#### (i) Matokeo ya Ukaguzi Maalumu Bodi ya Pamba Tanzania (TCB)

Ukaguzi maalum wa Bodi ya Pamba Tanzania ulibaini masula mbalimbali ikiwemo yafuatayo:

- Bodi hiyo ilipata hasara ya Shilingi milioni 166.45 ikiwa ni kiasi kilicholipwa zaidi ya kilichostahili kulipwa kwa kampuni zinazonunua pamba.
- Ruzuku ya kiasi cha Shilingi milioni 68.73 hakikulipwa kwa wakulima wa pamba na kampuni ya S & G wakati fedha hizo zilikuwa zimekwishakulipwa kwa kampuni hiyo na Bodi ya Pamba.
- Kampuni za Badugu Ginning Company Ltd na Vearrian (T) zilifunga na kusitisha biashara ya ununuzi wa pamba kabla ya kuwalipa wakulima wa pamba stahili zao za ruzuku ya kiasi cha Shilingi milioni 105.82.
- Ilibainiki pia, kiasi cha ruzuku ya Shilingi milioni 104.68 hakikulipwa kwa wakulima wa pamba kutokana na kupoteza stakabadhi za mauzo ya pamba na kukosa vielelezo vya kulipwa ruzuku hiyo. Hata hivyo kiasi hicho cha fedha bado hakijareshwa Hazina na Bodi ya Pamba Tanzania.




**(ii) Matokeo ya Ukaguzi Maalum Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya(MBEUWSA)**


Katika ukaguzi maalum wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEUWSA),yalibainika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo

- Kiasi cha Shilingi Milioni 554.60 kilitumika kununua mita za maji lakini haikujulikana idadi ya mita zilizonunuliwa kwa fedha hizo licha ya kuwa wateja 2,399 wanaopata huduma ya maji kutoka kwa Mamlaka hiyo hawakuwa wamefungiwa mita za maji.
- Watumishi 30 walioajiriwa na Mamlaka hiyo bila ya kutangaza nafasi hizo kinyume na utaratibu wa ajira wa Mamlaka, ikiwa ni pamoja na watumishi watano walioajiriwa na Mamlaka na kupewa mishahara mikubwa ambayo haikuendena na nafasi zao kinyume na ikama ya Mamlaka.
- Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa udhaifu katika udhibiti wa hati za madai ambapo kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2012 hati zenye thamani ya jumla ya Shilingi milioni 155.3 hazikuingizwa kwenye mfumo wa kompyuta unaotumiwa na Mamlaka.
- Mamlaka ilibainika kuwa na mgongano wa kimaslahi katika ununuzi ambapo kampuni ya Transportation Agricultural and Milling Services inayomilikiwa na Mkuu wa Kitengo cha Fedha ilibainika kufanya biashara na Mamlaka.
- Pia Mamlaka ilifanya malipo ya kiasi cha Shilingi milioni 70.1 bila ya kuwepo kwa Ankara za madai ili kuhakiki kama malipo hayo yalikuwa sahihi.

**(iii) Matokeo ya Ukaguzi Maalumu Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)**

- Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa uangalizi sio madhubuti kutoka kwa Menejimenti ya kampuni kwenye maandalizi ya mishahara ambapo

mtumishi mmoja aliweza kuiba kwa kujizidishia mshahara wake kwa kiasi cha Shilingi Milioni 71.77. Kiasi hicho kiliingia kwenye akaunti yake ya benki zaidi ya mshahara wake wa kawaida.




- Pia ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Sheria ya ununuzi haikuzingatiwa vyema katika ununuzi wa Bajaji 30 zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 156 na ununuzi ya magari 10 yenye thamani ya Shi lingi Bilioni 1.25. Kwa upande mwingine ukaguzi ulibaini kuwa Kampuni ya simu Tanzania (TTCL) haikuweza kudhibiti vizuri matumizi ya mafuta ya magari hali iliyopelekea kampuni hiyo kupata hasara ya Shilingi Milioni 73.97.

## SURA YA TISA

## UKAGUZI WA UFANISI

### 9.0 UTANGULIZI

Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kifungu cha 28 kinampa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi. Lengo la ukaguzi huu ni kutoa tathmini ya kiwango ambacho taasisi ya serikali inatumia rasilimali zake katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Vigezo mbali mbali hutumika katika kuchagua maeneo ya kufanya ukaguzi wa ufanisi ikiwa ni pamoja na malalamiko kutoka kwa wananchi na umuhimu wa eneo husika kwa sababu za kiuchumi au kijamii.

Sura hii inatoa muhtasari wa taarifa za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika hadi kufikia Machi 31, 2015 na kuwasilishwa bungeni kama ifuatavyo:

(i) Usimamizi wa Mipango Miji,
(ii) Ukarabati wa Majengo ya Serikali,
(iii) Makisio ya Mahitaji na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba Muhimu.
(iv) Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima Tanzania,na
(v) Utekelezaji wa Mifumo ya Utunzaji wa Mazingira kwenye Sekta ya Madini.

Malengo ya kaguzi hizi ni kutoa tathmini ya jinsi Serikali inavyotoa huduma katika maeneo tajwa hapo juu kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Ufuatao ni muhtasari wa kaguzi tajwa.

### 9.1 USIMAMIZI WA MIPANGO MIJI

***Sababu za kufanya ukaguzi***

Hali ya mipango miji nchini si ya kuridhisha. Ongezeko la watu wanaoishi katika maeneo ya miji linasababisha kuongezeka kwa ujenzi holela siku hadi siku na kupelekea ukosefu wa huduma muhimu. Pia inahatarisha ustawi wa wakazi na uendelezaji wa miji kwa ujumla. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi wa ufanisi kuangalia jinsi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) wanavyosimamia shughuli za mipango miji nchini.

## Lengo la Ukaguzi

- Kuangalia kama mifumo ya Mipango Miji inasimamiwa ipasavyo

## Mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi

- Asilimia 80 ya miji inaendelezwa bila ya kuwa na mipango kabambe (*master plan*) inayotoa muongozo wa uendelezaji wa miji hiyo;
- Miji yenye mipango kabambe, inaudhaifu katika utekelezaji wake. kwa Mfano maeneo yaliyopangwa kwa shughuli za viwanda na misitu yanatumika kwa makazi;
- Mikakati ya mipango miji haijikiti katika kuandaa ramani za mipango miji;
- Ushirikishwaji mdogo wa wadau muhimu wanaohusika na utekelezaji wa mipango kabambe; na
- Udhaifu katika kufuatilia na kutathmini shughuli za mipango miji nchini.

## Madhara

- Kukithiri kwa ujenzi holela wa makazi unaosababisha uchafuzi wa mazingira, ugumu katika uwekaji wa miundombinu ya barabara na ya huduma kama maji safi na taka na umeme;
- Inasababisha uwepo wa foleni barabara kwa miji mikubwa; na
- Inazuia ufanisi wa Jeshi la Zimamoto na uokoaji katika kufanya kazi zake.

## Hitimisho

- Sekta ya mipango miji haisimamiwi ipasavyo kwani miji mingi nchini inaongozwa bila ya kufuata "*master* plan" ya wakati husika.

## Mapendekezo

- Mipango miji itambuliwe kama eneo la kipaumbele katika ngazi ya taifa na Serikali za Mitaa;
- Kila mji uwe na Mpango kabambe na ufanyiwe marekebisho kama taratibu zinavyotaka;
- Kipaumbele cha mikakati ya mipango miji kiwe uandaaji wa mpango kabambe;
- Shughuli za mipango miji zifuatiliwe na zitathminiwe kwa ukaribu; na
- Kuwepo na uratibu mzuri wa wadau katika shughuli yoyote ya maendeleo

## 9.2 MAKISIO YA MAHITAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA MUHIMU

**Sababu za kufanya ukaguzi**

Kumekuwepo malalamiko kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali wa sekta ya afya nchini juu ya uhaba wa dawa na vifaa tiba muhimu. Tatizo limeendelea kuwepo licha ya maboresho kadhaa yaliyofanywa na Serikali. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi kuangalia jinsi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Bohari Kuu ya Dawa inavyosimamia shughuli hiyo.

**Lengo la Ukaguzi**

Kutathmini kama makisio ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba muhimu pamoja na usambazaji wake unalenga kupunguza tatizo la uhaba wa dawa na vifaa tiba muhimu katika vituo vya afya.

**Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi**

- Tathmini ya makadirio ya uhitaji siyo ya uhakika;
- Muda mrefu wa kuandaa na kusambaza oda ya dawa na vifaa tiba muhimu;
- Mfumo dhaifu wa ufuatiliaji na tathmini ya usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu; na
- Upatikanaji wa fedha usio madhubuti na uhakika.

**Hitimisho**

- Shughuli za makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu hazisimamiwi ipasavyo kuhakikisha upatikanaji wake katika vituo vya afya kama inavyotakiwa.

**Madhara**

- Wananchi kukosa huduma za afya za uhakika kutokana na ukosefu wa dawa na vifaa tiba muhimu; na
- Ongezeko la gharama za huduma za afya na vifaa tiba muhimu pale wananchi wanapokosa huduma hizo kwenye vituo vya afya vya serikali.

**Mapendekezo**

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Bohari Kuu ya Dawa itathmini hali ya mtaji wa uendeshaji na mfumo mzima wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu kwa lengo la kutatua tatizo la uhaba wa dawa na vifaa tiba muhimu.

## 9.3 UKARABATI WA MAJENGO YA SERIKALI

***Sababu za kufanya ukaguzi***

Majengo ya serikali yamekuwa hayafanyiwi ukarabati wa mara kwa mara. Hii imefanya kuwepo kwa mazingira yasiyo salama ya sehemu za kazi/malazi kwa wafanyakazi wa serikali. Baadhi ya majengo yamejengwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 20 hadi 80 iliyopita bila ya ukarabati. Hali hiyo iliifanya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya Ukaguzi wa ufanisi kuangalia jinsi Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Majengo nchini inavyosimamia eneo hilo.

**Lengo la Ukaguzi**

Kutathmini ufanisi wa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Majengo nchini katika kusimamia ukarabati wa Majengo ya Serikali.

**Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi**

- Udhaifu katika utekelezaji wa shughuli za ukarabati wa majengo;
- Mipango duni ya ukarabati wa majengo ya serikali; na
- Mfumo dhaifu wa kutathmini na kufuatilia shughuli ya ukarabati wa majengo ya serikali.

**Hitimisho**

Shughuli za ukarabati wa majengo ya serikali hazisimamiwi ipasavyo.

**Madhara**

Majengo ya serikali kuendelea kuwa katika hali duni hivyo kuhatarisha usalama wa kazi na watumiaji wa majengo hayo.

**Mapendekezo**

Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Majengo nchini ziandae Sera ya ukarabati wa majengo yanayomilikiwa na serikali na kufuatilia utekelezaji wake. Hii ni pamoja na kuweka kumbukumbu sahihi ya majengo hayo.

## 9.4 UTOAJI WA HUDUMA ZA UGANI KWA WAKULIMA

***Sababu ya kufanya ukaguzi***

Ingawa zaidi ya asilimia 80 ya watanzania wanajishughulisha na kilimo, hali ya uzalishaji katika sekta hiyo inashuka. Hii inatokea licha ya Serikali kuanzisha programu ya huduma za ugani katika shughuli za kilimo. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi wa ufanisi kuangalia jinsi Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na OWM-TAMISEMI wanavyosimamia huduma za ugani kwa wakulima.

**Lengo la Ukaguzi**

Kutathmini namna shughuli za ugani kwa wakulima zinavyosimamiwa nchini.

**Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi**

- Mapungufu katika uboreshaji wa teknolojia za kilimo;
- Ucheleweshwaji wa fedha na kusababisha huduma duni za ugani;
- Utoaji duni wa huduma za ugani kutokana na ukosefu wa miongozo; na
- Ufuatiliaji duni wa utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima.

**Hitimisho**

Usimamizi wa shughuli za utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima nchini ni dhaifu.

**Madhara**

- Shughuli za huduma ya ugani kwa wakulima kutokuwa na tija
- Uzalishaji mdogo katika shughuli za kilimo kutokana na elimu duni ya kilimo

**Mapendekezo**

- Ifanyike tathmini namna ya kuboresha teknolojia za kilimo ili kuongeza tija katika shughuli za kilimo.
- Fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za ugani zitolewe na zitumike kwa shughuli husika.
- Kuwe na ufuatiliaji makini juu ya utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima

## 9.5 UTEKELEZAJI WA MIFUMO YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA KWENYE SEKTA YA MADINI

***Sababu ya kufanya ukaguzi***

Shughuli za uchimbaji wa madini zinaendelea kufanywa maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali juu ya uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli hizo. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi wa ufanisi kuangalia jinsi Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira wanavyosimamia shughuli za mazingira nchini.

**Lengo la Ukaguzi**

Kutathmini uandaaji wa mipango na usimamizi wa utekelezaji wa mifumo ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika shughuli za uchimbaji madini.

**Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi**

- Mipango isiyojitosheleza ya usimamizi wa mazingira;
- Usimamizi mdogo wa adhabu zilizopo;
- Taarifa za usimamizi wa mazingira kutotolewa kwa wakati na kwa kiwango kinachoridhisha;
- Kukosekana kwa uratibu makini wa shughuli za usimamizi wa mazingira;na
- Kaguzi za mazingira zinazofuatilia utekelezaji wa masharti yaliyowekwa kwa wachimabaji madini kutokuwa na ubora .

**Hitimisho**

Usimamizi wa mazingira kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini nchini ni dhaifu.

**Madhara**

Maeneo yanayozungukwa na sehemu zenye shughuli za uchimbaji wa madini ni hatarishi kwa ustawi jamii na viumbe hai.

**Mapendekezo**

- Adhabu stahiki zitolewe kwa wanaobainika kuvunja sheria;
- Kuwe na ufuatiliaji wa utekelezaji wa masharti yaliyotolewa wakati wa ukaguzi wa awali wa athari za mazingira; na
- Kuwe na ufuatiliaji wa utendaji kazi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

# SURA YA KUMI

## 10.0 MAONI MAALUM YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kwa mujibu wa Kifungu 12 cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ningependa kutoa mapendekezo kwa mambo mengine ambapo kama yatatekelezwa itasaidia kuzuia au kupunguza masuala yasiyo na tija katika matumizi ya rasilimali za serikali. Hivyo basi, napenda kuishauri Serikali katika maeneo yafuatayo:

### 10.1 Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kuwepo kwa udhaifu katika kusimamia matumizi ya ardhi umepelekea kuongezeka kwa makazi yasiyopimwa katika maeneo ya mijini na hivyo kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa inapotaka kujenga miundombinu kama barabara, miundombinu ya maji n.k. Katika Mwaka wa ukaguzi unaoishia 2013/2014 Mkoa wa Dodoma umechukuliwa kama mfano ambao ulikuwa na migogoro kumi na tatu (13) inayohusiana na mipaka kati ya Wilaya, Vijiji na Hifadhi za Taifa.

Kwa Halmashauri za Manispaa tatu za Temeke, Ilala na Kinondoni zilichukuliwa pia kuwakilisha Halmashauri nyingine na zilikuwa na zaidi ya kesi za ardhi 74 ambazo sababu zake karibu ni zile zilizoelezwa katika Sera ya Ardhi ya Taifa. Kwa kuzingitia migogoro hiyo nashauri yafuatayo:

(a) Serikali itayarishe mpango mkakati wa muda mfupi na mrefu kukabiliana na migogoro ya ardhi inayoongezeka kwa kuzingatia Sheria na Sera zilizopo,

(b) Serikali iimarishe usimamizi wa Sheria na Kanuni za Ardhi, na ishirikishe jamii katika usimamizi wa matumizi ya ardhi kwa kuwajengea uelewa, na

(c) Kupanga na kupima mapema maeneo yanayoonekana kuvutia watu kwa makazi, uwekezaji au kuendesha shughuli za kiuchumi kabla ya migogoro kutokea.

### 10.2 Changamoto kuhusiana na uanzishwaji wa Halmashauri Mpya.

Katika mwaka wa fedha 2013/14, Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 zilianzishwa na zote zilikaguliwa. Hata hivyo, kulikuwa na changamoto zilizoonekana katika uanzishwaji huo ambazo ni:

i. Uhaba mkubwa wa miundombinu katika makao makuu mpya ya halmashauri hususani majengo ya ofisi na nyumba za watumishi.
ii. Upungufu wa watumishi wakuu na uwepo wa Watumishi wanaokaimu kwa muda Mrefu.
iii. Kutokuwepo kwa miongozo ya kutosha katika uandaaji wa taarifa za fedha hususani jinsi ya kuripoti mali za kudumu; na kutotunza vizuri Kumbukumbu za Mali za Kudumu na Madeni kabla ya kugawanyika kwa halmashauri.
iv. Kutokuwepo kwa mfumo wa kompyuter kwa kazi za uhasibu.

Tunashauri Serikali kutambua na kupanga mapema namna ya kupunguza changamoto zitokanazo na uanzishwaji wa Halmashauri hizo kabla ya Kuanzishwa.